



JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA BUHIGWE

Simu fax:+255 0282910 339

Barua pepe:ded@buhigwec.tamisemi.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

S.L.P 443

BUHIGWE

20 Desemba, 2021.

M.P/H

TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe kwa shirikiana shirika la Tanzania Health Promotion Support (THPS) inatangza nafasi za kazi za mkataba.

A.Mtaalamu wa kutoa huduma za Matibabu na Matunzo kwa WAVIU kwa kutumia tanzidata (CTC2 database) –(Nafasi 1)

KURIPOTI KWA: Mganga Mkuu Wilaya.

KITUO CHA KAZI:Zahanati ya Mugera.

Majukumu atakayotekeleza

Atakuwa kama mtumishi wa kituo husika kwa kufanya majukumu yafuatayo:-

- i. Kuhakikisha utoaji huduma kwa wateja wa kliniki ya matunzo na matibabu kwa kila siku.
- ii. Kuhakikisha faili za wateja zinapatikana siku moja kabla ya siku ya kliniki.
- iii. Kuhakikisha kituo kinafikia malengo yaliyowekwa kwa kutoa huduma bora kwa wateja wanaoanza dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI na wale wengine wanaoendelea.
- iv. Kuhakikisha 75% ya wateja wote walio na vigezo vya kuchukua dawa za miezi za 6 na miezi 3 wanapata dawa.
- v. Kuhakikisha takwimu zilizo sahihi zinaingizwa kwenye mfumo.(CTC2 database)
- vi. Kufundisha timu juu ya matumizi ya takwimu.
- vii. Kupakuwa taarifa kila siku kutoka CTC2 database,Data analytics, macro3 na DHIS2.

Majukumu yote utayopangiwa na mkuu wa kazi

SIFA ZA MUOMBAJI:

- i. Awe na elimu ya kuanzia kidato cha nne.
- ii. Awe muuguzi.
- iii. Awe na leseni hai.
- iv. Awe na ujuzi wa kutumia komputa (Ms Word, Excel, and Access).
- v. Awe na uwezo wa kutumia CTC2 database,Data analytics Companion, macro3 na DHIS2.
- vi. Uwezo wa kuongea,kusoma na kuandika Kiswahili and Kiingereza.

B.AFISA TAKWIMU (Nafasi 1)

KITUO CHA KAZI: Kituo cha Afya Munzeze.

RIPOTI KWA: Mganga Mkuu wilaya.

Majukumu atayotekeleza

- i. Kuhakikisha takwimu zilizo sahihi zinaingizwa kwenye mfumo.
- ii. Kufundisha timu juu ya matumizi ya takwimu.
- iii. Kupakuwa taarifa kila siku kutoka CTC2 database, Data analytics, macro3 na DHIS2.
- iv. Majukumu yote utayopangiwa na mkuu wa kazi.

SIFA YA MUOMBAJI:

1. Shahada au Stashahada ya juu kwa kozi ya komputa .
2. Awe na uzoefu angalau miaka 3 katika masuala ya takwimu.
3. Awe na uwezo wa kutumia MS Access.
4. Awe na uwezo wa kuandika na kuongea Kingereza na Kiswahili.
5. Awe na uwezo wa kuandaa ripoti na kutumia kanzidata mbalimbali (Micro3, CTC2 databases)

Mwisho wa kupokea maombi ni Tarehe 28 Desemba, 2021 saa 9.30 Alasiri.

Maombi yote yatume kwa Anuani kwa:-


Mkurugenzi Mtendaji(W),

S.L.P. 443,

BUHIGWE.

Limetolewa na

PP 
Essau H. Ngoloka
Mkurugenzi Mtendaji
BUHIGWE



*Neu
MFTA*